CHUO KIKUU CHA
MT. AGUSTINO CHA TANZANIA

SALAMU ZA POLE

Mhashamu Baba Askofu Wolfgang Pisa OFMCap, Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania (St. Augustine University of Tanzania-SAUT), anasikitika kutangaza kifo cha **Mhashamu Baba Askofu Bernadini Francis Mfumbusa, Askofu wa Jimbo Katoliki Kondoa**, kilichotokea tarehe **14 Aprili 2026,** alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Benjamini Mkapa, Dodoma.

Kwa namna ya kipekee, jumuiya ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania (SAUT) itamkumbuka Askofu Mfumbusa kama Mhadhiri mwandamizi aliyehudumu katika Idara ya Mawasiliano ya Umma kuanzia mwaka 1999 hadi 2011. Aidha, aliteuliwa kuwa Mkuu wa Idara hiyo mwaka 2004 hadi 2005. Vilevile, alihudumu kama Mkuu wa Kitivo cha Sayansi ya Jamii na Mawasiliano mwaka 2005 hadi 2007. Kutokana na utendaji wake uliotukuka na wenye maono thabiti, aliteuliwa kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma kuanzia mwaka 2007 hadi 2011, kabla ya kuteuliwa na Baba Mtakatifu kuwa Askofu wa Kwanza wa Jimbo Katoliki Kondoa.

Jumuiya ya SAUT itaendelea kumkumbuka Askofu Mfumbusa kwa mchango wake mkubwa katika tafiti mbalimbali pamoja na huduma yake kwa Kanisa.

Kwa niaba ya jumuiya ya Chuo Kikuu cha SAUT, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Padri Prof. Juvenalis Asantemungu anatoa pole za dhati kwa Familia ya Marehemu, Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Ndugu, Jamaa na Marafiki kwa msiba huu mkubwa.

Ibada ya Misa Takatifu ya mazishi pamoja na maziko itafanyika tarehe 22 Aprili 2026 katika Kanisa la Roho Mtakatifu, Jimbo la Kondoa, kuanzia saa 4:00 asubuhi.

Tunaomba tuendelee kumwombea Marehemu Pumziko la Amani

"Raha ya Milele Umpe Ee Bwana, na Mwanga wa Milele Umwangazie.
Apumzike kwa Amani. Amina"

Padri Prof. Juvenalis Asantemungu
Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo